

NILIMDHANIA KAHABA KUMBE BIKRA

MTUNZI: SINGANOJR

Mono no aware.

SEHEMU YA 680.

Kila mtu alishangaa mara baada ya Clark kusema kilichompata Yezi ni sumu , haikueleweka sumu hio imetokea wapi.

Yezi asingeenda mbali hivyo kunywa sumu kwasababu tu hataki ndoa hivyo moja kwa moja kila mtu alijua amewekewa sumu.

Clark hakujisumbua hata kutoa majibu kwa Park Juan na kwa watu waliokuwa wakitaka maelezo.

“Hubby mtoe Yezi hapa tumpeleke sehemu tulivu” Aliongea Clark.

Roma hakutaka kujali chochote na palepale alimbeba Yezi na kwenda kumpeleka kwenye moja wapo ya

vyumba vilivyokuwa ndani ya eneo hilo huku Clark akimfuata kwa nyuma.

“Kulingana na uzoefu wangu pamoja na uelewa , dalili zinaonyesha sumu ni Pottassium cyanide , ni sumu ambayo inasharabu maji na Carbondioxide na kudhalisha gesi ya Hydrogen cyanide , inasababisha mwili kukakamaaa , shida ya kupumua na kuzuia mzunguko wa damu mpaka kupelekea kifo”Aliongea Clark na Roma palepale alimuweka Yezi kwenye Sofa.

Alikuwa akitetemeka pamoja na kukamaa mfululizo na macho yake yalikuwa yamechomoza nje.

“Sijali ni sumu ya aina gani , niambie ni kwa namna gani tunaweza kumuokoa”

“Tushachelewa kwa matibabu ya dharula , Hubby kwanini usitumie mbinu yako ya kijini ya andiko la urejesho pamoja na vidonge kumwingizia nguvu ya kijini ndani ya mwili wake na kuimarisha seli za mwili , zikishakuwa na nguvu itakuwa rahisi ku'metabolize' na kutoa sumu mwilini”Aliongea Clark.

Roma alijua hana muda wa kufikiria kwa wakati huo , alishawahi kumtoa mtu sumu mwilini lakini kuhusu sumu hio ilikuwa kali sana.

Dakika ileile alitoa kidonge alichotengeneza kupitia mifupa ya majini Joka na mimea na kisha akamlisha Yezi.

Kidonge cha aina hio kazi yake ilikuwa ni kuimarisha mwili lakini pia kurahisisha nguvu ya kijini kufanya kazi ndani ya mwili , baada ya kufanya hivyo palepale alianza kumwingizia nguvu ya andiko kuyeyusha kile kidonge ili kuingia katika mzunguko wa damu.

Muda huo kundi lote la wageni likiongozwa na babu yake Yezi walikuwa washakifka mlangoni na Clark aliwazuia kwa nje.

“Sir kama unatuamini tafadhari usiingie ndani au vinginevyo utalipia gharama za kumpoteza mjukuu wako”Aliongea kibabe huku akitoa ile Aura ya kuogopeka.

Park Juan alijikuta akirudi nyuma kwa hofu kidogo , lakini alikumbuka uwezo wa Clark katika matibabu pamoja na mbinu za Roma za kimaajabu ,alijikuta

akitulia kidogo na kisha kung'ata meno kwa hasira na kukinga wengine.

“Okey kama dokta alivyosema hakuna anaeruhusiwa kuingia”

Mabodigadi muda uleule walizingira eneo lote kutoruhusu mtu na wageni walianza kuondoka mmoja mmoja.

“Sir natoa ushauri wa kuzuia watu wasiondoke ndani ya eneo lote ambalo Yezi alikuwepo , kila mmoja hapa ni mtuhumiwa , baada ya Yezi kutoka katika hatari tunapaswa kumkamata muhusika” Aliongea Clark na kumfanya Park Juan palepale kuelewa na kutoa maagizo kwa watu wake kufanya kazi hio.

“Dr Clark Yezi ndio uhai wangu... tafadhari naomba muokoeni”

Aliongea Park Juan akiwa amepiga magoti mbele ya Clark na palepale Clark alimzuia na kumfariji.

“Usiwe na wasiwasi , kulingana na nilichoona dozi ya sumu iliompata ni kidogo sana ndio maana hajafa hapo hapo , kuna matumaini makubwa ya kupona”

Clark hakutaka kumpa matumaini makubwa, isitoshe sumu kama Potassium Cyanide ilikuwa ni hatari na asingeweza kumsaidia kama asingekuwepo Roma.

Inaonekana aliedhamiria kufanya jambo hilo alikuwa amenuia kumuua kabisa.

“Sir nitahitafi vifaa na baadhi ya dawa , najua mtu ndani ya taasisi moja ya kikemia hapa nchini naomba umwagize mtu anisaidie kuvileta” Aliongea na Park Juan hakuuliza mara mbilimbili na alikubali maagizo yake.

Muda nao ulisogea , ile hali ya furaha na shangwe iliokuwa imetegemewa ilikuwa imepotea na wahudumu waliopangwa kwa ajili ya sherehe hio walikuwa wamejikusanya sehemu moja huku kila mmoja akiwa na mwonekano usiokuwa ukielezeka.

Wageni pia hakuna ambaye aliruhusiwa kuondoka , kuna ambao walikuwa wakiombea kupona kwa Yezi lakini pia kuna wale waliokuwa wakiombea kutopona kwake.

Lakini wote walionekana kuwa na shauku ya kutaka kupata taarifa ya kile kinachoendelea .

Ndani ya chumba katika sofa Roma alikuwa bize kuondoa sumu mwilini kwa spidi kubwa, na kila anapofanya mwili wa Yezi uliota vipele vikubwa kwenye ngozi yake ambavyo vilikuwa vimejaa damu nyeusi mpaka anakuja kumaliza raundi ya mwisho alijikuta akivuta pumzi nyingi ya ahueni.

Roma alipatwa na ahueni mara baada ya kuona sasa Yezi alikuwa akipumua vizuri na rangi yake ya uso ilikuwa imemrudia ikimaanisha mzunguko wa damu ushaanza kufanya kazi.

Baada ya hatua ya awali kukamilika alimwingizia Yezi nguvu ya kijini na kisha kuibadilisha kuwa maji ya kiroho na yakaanza kusafisha sumu yote mwilini na ndani ya dakika chache tu vile vipele vilianza kupotea.

Clark aliekuwa akilinda mlangoni alijikuta akivuta pumzi yaa hueni mara baada ya kuona mafanikio hayo.

“Asante Mungu ulikuwepo leo na pia umerudiwa na nguvu zako , la sivyo Yezi angekufa”Aliongea Clark mara baada ya kuona Roma sasa amemaliza.

Roma aliishia kushika mashavu ya Yezi na kurudisha nywele zake nyuma, ilipaswa kuwa harusi yake lakini ndio hivyo kidogo tu afe.

Kitendo cha kuhisi kuna mtu ambaye alitaka kumuua Yezi kilifanya macho yake kutokuwa ya kawaida kabisa.

“Ulienda kufanya utafiti katika eneo la tukio?”

“Yeah , nimegunfdua namna tukio lilivyofanyika lakini sijampata muhusika bado”

“Hawawezi kufanya hivi bila ya kuhudhuria sherehe , muhusika lazima atakuwa ni mtu ndani ya hili eneo , tuwachunguze wote mmoja mmoja nina uhakika tutampata” Aliongea Roma na wote kwa pamoja walitoka.

Baada ya taarifa kutolewa kwamba Yezi ametoka katika hatari ya kifo Park nJuan alifurahi sana na kumshukuru Roma kwa kazi yake.

“Mr Roma naruhusiwe kwenda kumuona Yezi?” Aliuliza Park Juan.

“Hapana , kila mtu ndani ya hili eneo ni mtuhumiwa mpaka pale tutakapo pata muhusika mwenyewe ,hiyo

nazuia mtu yoyote kusogea karibu na chumba alipo Yezi”Aliongea Roma kwa Kikorea na kufanya kila mmoja hapo ndani kutofurahishwa na kauli yake.

“Wewe ni nani , kwanini tukusikilize?” Bwana mmoja alionekna kama kiongozi aliongea huku akionyesha kejeli , alijiambia kwanini amsikilize mtu mweusi.

“Kama unajiamini sogea uone , nitakukuchukulia kama mtuhimiwa mkuu namba moja”Aliongea Roma kibabe na kufanya watu wote kumwangalia kwa macho ya wasiwasi.

Yule bwana hakutaka kuleta fujo , pengine aliogopa Roma alivyokuwa akiongea na kujjiamini na alikosa ujasiri wa kujibishana nae.

Hakuna mgeni ambaye alitaka kuchukuliwa kama mhalifu hivyo moja kwa moja walitulia katika eneo walioelekezwa.,

Dakika hio hio Clark alisogea akiwa ameshikilia Shera ambayo alikuwa ameivaa Yezi na kuwaonyesha watu wote.

“Jamani hebu angalieni , hii shera ndio imetumika kumuwekea Sumu Yezi , mtuhumiwa alichokifanya ni kupaka hii shera na sumu aina ya Pottasium

Cyanide , wakati Yezi alipokuwa akipumua ule unyevu nyevu wa maji uligusana na Pottasium Cyanide na kugeuka gesi aina ya Hydrogen Cyanide ambayo ni sumu kali inapoingia kwenye mapafu, nimeulizia na kuambiwa gauni la harusi halikupewa ulinzi wala umakini wa ki usalama hivyo kutoa nafasi kwa mgeni yoyote yule kulishika wakati lilipokuwa linapelekwa kwa bibi harusi , hivyo mtu yoyote anaweza akafanya hili tukio , tunaomba ushirikiano wenu kumkamata mhalifu”

“Hakuna mtu yoyote ambaye anaruhusiwa kuondoka hili eneo mpaka uchunguzi ukamilike , wale wote ambao wana kinyongo na familia ya Park aidha ni zamani au sasa hivi naomba msogee mbele”Aliongea Roma.

“Unatania wewe katika swala muhiu kama hili , kama ni kuanza anza na wahudumu kwanza na wahusika waliompaka Make up , ndio wahusika wa kimantiki acha kupoteza muda na sisi”Alibweka mkorea mmoja.

“Sitaki unifundishe chakufanya , hata wao pia watafanyiwa uchunguzi isitoshe kwanini waweke Shera sumu ilihali watakuwa wahusika wa

kwanza?” Aliuliza Roma na kufanya wageni wote kuona ana mantiki.

“Kama unataka kujua ni nani ambaye ana kinyongo na familia ya Park basi itakuwa ni familia ya Gong Gyechung” Alionga mgeni mmoja na kumfanya Gong Gyechung na Gong Woo kumwangalia kwa macho makali.

“Hatuwezi kufanya kitu cha kijinga kama hichi, Yezi anaweza akawa amemkataa mtoto wangu lakini baba yangu alikuwa ni mtu wa karibu na Mzee Park, familia zetu ni kama ndugu”

“Hakuna ambaye anaweza kuamini, kila mmoja anajua ulitaka Mzee Park kuendelea kuugua wakati huo ukimfanya mtoto wako kumuoa Yezi ili ukwapue mali zake”

Muda kama huo kila mgeni alitaka kuondokana na tatizo hilo na kwasababu Park Juan alikuwa amekasirika ilikuwa rahisi kubebesha mzigo familia nyingine.

Gong Gyechung na ndugu zake wote walijua kabisa wao ndio washukiwa namna moja kutokana na

matukio yaliopita , ilikuwa ni sawa kusema wana sababu za msingi kufanya tukio kama hilo.

“Hatuhusiki , baba haina haja ya kujibizana nao na hakuna ambaye ana uthubutu wa kutuzuia kutoondoa apa” Aliongea Gong Woo huku akimwangalia Roma kwa hasira.

“Upo sahihi mwanangu , nyie watu hapa wote ni kama mbwa kichaa tu na mnachofanya ni kutaka kunibebesha lawama mimi na familia yangu ili kujiokoa , hivi mnadhani tunaogopa?”

“Halafu tunaruhusije mtu kutoka mataifa yanayoendelea kutuamulia maswala yetu , acheni kuongea upumbavu nitapigia simu polisi waje wamuweke polisi”

Baada ya kuongea vile kila mmoja alikumbushwa nafasi yake katika jamii,ni kweli waliokuwepo hapo ndani ni watu kutoka mataifa mbalimbali ndani ya Asia ambao wana ukwasi mkubwa wa pesa , kwannini wamsikilize mtu mweusi, isitoshe hata kuhudhuria kwao ni kwa ajili ya heshima kwa Park Juan tu.

Gong Gyechung na ndugu zake walianza kuomba kupishwa njia kuondoka ndani ya eneo hilo.

Upande wa wageni na wenyewe walianza kujidharau kwa kukubali maneno ya mtu mweusi kama Roma na waliishia kumwangalia Roma kwa macho ya kejeli.

Park Juan mwenyewe alishajua kuhusu hilo kulikuwa na watu wazito ndani ya hilo eneo na matajiri kuliko hata yeye mwenyewe na ni ngumu kukubali kuonyesha ushirikiano.

Kundi lote lilianza kutafuta njia ya kuondoka , huku wengine wakianza kupanga mipango ya kukutana kwa ajili ya chakula makusudi kabisa wakionyesha kuchukizwa na Roma

Lakini sasa Roma alionekana kutopendezwa na dharau zao na palepale alienda kuwazuia Gong Gyechung na familia yake kwa mbele.

“Unafanya nini? , hujui kwamba hii ni nchi inayoendeshwa kisheria , tutakufunga kwa kutuingilia ndani ya nchi yetu”Aliongea Gong Gyechung kibabe.

Roma hakujali maneno yake na palepale alisogea mpaka karibu na mlango wa kutokea na alipasua Chandelias kubwa iliokuwa imening'inizwa.

Kwa namna alivyoruka mpaka kuipasua na kuja kutua chini ilifanya wale wageni kurudi nyuma kwa hofu na hata Park Juan mwenyewe alijikuta akipatwa na hofu.

Roma hakuishia kwenye kupasua tu ile Chandelina palepale alianza kusambaza nguvu ya kijini ya kutia watu uoga na kufanya kila mtu kushindwa kupiga hatua na hata wale ambao walikuwa wakimwangalia kwa Dhara walianza kuona woga.

“Nitaanza na nyie” Aliongea Roma na palepale alimshika Gong Gyechung pamoja na Gong Woo na kuwarushia katikati kama mafurushi na kisha alimpa ishara Clark kuwaagiza mabodigadi kuwakagua.

Walikaguliwa wote kwa haraka haraka na wale mabodigadi na Clark pia alifanya baadhi ya vipimo vya kikemikali na aliona kila kitu kipo sawa.

“Sio wahusika” Aliongea Clark na palepale Roma aligeukia wageni wengine.

“Kama nilivyosema wale wote wenye uadui na kinyongo na familia ya Park watoke mbele” Aliongea Roma huku akisambaza hali ya woga na kila mtu

hapo ndani alimuona kama Simba na watu zaidi ya kumi na mbili walitoka mbele.

Clark aliwakagua wote lakini hakuna ambaye alkuwa ni muhusika na alionekana kushangaa .

“Hii inashangaza , kutokana na muda na namna tukio lilivyofanyika kama kweli walikuwa wakitaka kuweka sumu kwenye shera si lazima kuna poda ingebakia , au ni wahudumu ndio wamefanya?”

“Wote wapo hapa , hili eneo nimelizingira na nguvu za kijini na hakuna ambaye ametoka , kama hatuwezi kupata ushahidi kutoka kwao basi tutaanza kutafuta eneo lote” Aliongea na Clark alitingisha kichwa na kisha akamwambia Park Juan kuwajumuisha na wahudumu.

Lakini na wao wenyewe walikaguliwa na kufanyiwa vipimo na kifaa maalumu lakini hakuna ambaye alipatikana.

Muda huo huo Roma aligeuza macho yake kwa Eujung ambaye alikuwa amesimama pembeni ya Park Juan.

“Eujung wewe kazi yako ni kumhudumia Yezi , unapaswa kukaguliwa pia” Aliongea Roma na

kumfanya Park Juan na Mzee Km kumwalia Eujung kwa mshangao ni kama hawakuamini kama anaweza kufanya tukio la namna hio , isitoshe amekuwa karibu na Yezi kwa muda mrefu sana na alikuwa akimjali sana.

Eujung aliishia kulamba lipsi tu kuuva ujasiri na kisha alisogea mbele kwa ajili ya kukaguliwa.

Clark palepale kwa kutumia Gloves alianza kumkagua Eujung na kisha akachukua sample flani hivi kwenye nguo zake na kisha akaichanganya na kimiminika(Solution) chenye rangi ya maji lakini sasa baada ya kutingisha kwa dakika chache tu palepale rangi ilibadilika na kuwa pink na kumfanya Clark kutoa macho.

“Pottassium Cyanide , Eujung wewe ndio muhusika?”Aliuliza Clark kwa mshangao.

SEHEMU YA 681.

Kila mtu alishangazwa na kauli ya Clark na waliishia kumwangalia Eujung kwa mshangao mkubwa kana kwamba alikuwa akitegemea hilo , Eujung aliishia kung'ata lips zake za chini na kisha akainamisha kichwa chake chini bila ya kuongea neno.

Muda huo wageni wote walijikuta wakipatwa na ahueni kutokana na kwamba hawakuwa watuhumiwa tena kwasababu muhusika amekamatika.

“Inawezekanaje ,.... Kwanini awe ni Eujung?” Park Juan alijikuta akitetemeka huku akirudi nyuma kwa mshituko na macho yake yalibadilika palepale na kujawa na hasira.

“Wewe mwanaharamu , nini ambacho nilikukosea , kwanini ukamuwekea sumu Yezi?”

Kim Yang na Kim Jip waliishia kukunja sura tu huku wakimwangalia , Kim Jip alikuwa ni kama vile atalipuka muda wowote kutokana na hasira.

Roma muda huo aliishia kutulia sasa na kumwangalia Eujung akisubiria maelezo yake.

Eujung macho yake yalimvimba kutokana na kutoa machozi mengi na palepale aliinua uso wake huku akionyesha tabasamu la maumivu na aliishia kumeza mate huku akimwangalia Park Juan.

“Sir , naomba unisamehe lakini nimeisubiria hii siku kwa muda mrefu”

“Nini?” Aliuliza Park Juan kama vile hajamsikia vizuri.

“Nina uhakika ushamsahau mwanamke uliekutana nae miaka ishirini iliopita , jia lake anaitwa Ho Jiwan” Aliongea Eujung.

Park Juan palepale alijikuta akianza kutetemeka huku akiinua kidole chake akimnyooshea Eujung.

“Wewe ,,,, wewe ni ...”

“Ndio , Ho Jiwon ni mama yangu mzazi na mimi naitwa Ho Eujung”

“Hapana , haiwezekani , alisema alisema ,....”Park Juan alikuwa kama mtu ambaye anajaribu kuvuta kumbukumbu.

“Naona umeshindwa kuongea , basi nitakusaidia , kipindi kile wakati mama yangu akiwa msaidizi wako ulimtongoza ili kuwa mpenzi wako na mara baada ya kukubalia na kumpa mimba ulimwambia aitoe kwasababu uliogopa ingekuhabiria taswira yako , mama hakutaka kuitoa hivyo alikudanganya ameitoa na mimba ile ndio nilizaliwa mimi , mwanzoni alipanga baada ya mimi kuzaliwa kuja kukubembeleza ili unikubali lakini wewe ukampatia hela na kumfukuza ili kuzima uvumi uliokuwa ukiendelea ndani ya kampuni , hivi unajua hajawahi kutabasamu tokea siku ambayo amenizaa , alikuchukia kwasababu ulimtelekeza na alikuwa akinipiga kila saa na kunifokea akinilazmisha kupiga magoti na kuniongelea maneno ya laana , alikuwa ni mlevi wa kupindukia mpaka akapata saratani ya ya ini daraja la nne , nilikuja kugundua wewe ndio baba yangu wakati akiwa ndio anakaribia kufa ndio aliniambia kila kitu na kuniomba msamaha lakini

sikutaka kumlaumu , mtu ambaye namchukia ni wewe”

Aliongea Eujung huku akitoa kilio , kitendo cha kuzuia hisia zake na kuzitoa wakati huo ilimfanya kutikisika mabega kwa kulia.

Park Juan alijikuta akijikalia chini bila kujua , ni kama amezeeka na hajiwezi au ni kwasababu ya hatia ya matendo yake.

“Kwahio...kwahio ulikuja ndani ya familia yangu kwa ajili ya kulipiza kisasi?” Aliongea Park Juan huku akimwagalia mtoto wake wa kumzaa ambaye alikuwa amevalia mavazi ya kihudumu.

Mpaka hapo ilimaanisha kwamba ndio mtoto wake wa mwisho , Park Jiyeon na wadogo zake walikuwa katika hali mchanganyiko kwani hawakutegenea kijakazi wao amegeuka kuwa mdogo wao.

“Upo sahihi , nilijifunza Taekwondo na maswala ya kihudumu na ndio nikaingia kwenye familia yako , nilikuangalia siku zote na sura yako ya kinafiki na nimefikia hatua ya kumtaka mjukuu wako unaempenda kufa kwenye harusi yake , ninataka

ilimpie gharama kwa dhambi zako..”Aliongea kwa kufoka.

“Park Juan mapigo yake ya moyo yalikuwa yakidunda mno na kama sio kutumia vidonge vya Roma basi presha ingempanda.

“Mtoto wangu Eujung naomba nisamehe”Aliongea na kufanya kundi lote kushangaa kutokana na kitendo cha Park Juan kumkubalii kama mtoto wake.

“Eujung nimeshi kwa majuto sana kwa makosa ambayo nilifanya miaka mingi liopita , nilitamani kumtafuta mama yako na kumwomba msamaha lakini niliogopa namna ambavyo angeniangalia...Eujung naomba unisamehe mimi baba yako , nipo tayari kukupokea na kulipa fidia kwa miaka yote ambayo sikukutambua... Eujung mwannangu nipatie nafasi”Aliongea Park Juan.

“Acha kuwa mnafiki, uaniombaje nikupe nafasi ilihali nilitaka kumuua mjukuu wako na sumu?”Aliongea na ni kama Park Juan alishasahau na palepale alimgeukia Roma.

“Mr Roma tafadhari muachilie Eujung , alifanya haya yote kwasababu ananichukia na sio kwasababu anamchukia Yezi , kwasababu Yezi yupo salama naomba hili liishe na nakuahidi hiki kitendo hakitotokea tena....Eujung ni binti yangu na siwezi kuruhusu kumuona akifa mbele yangu”Aliongea kama vile alishajua mpango wa Roma ni kumuua muhusika.

“Mimi sitaku unafiki wako , nipo tayari kufa , naomba umuache Mr Roma anue hapa hapa , hio ndio njia pekee ya kunifanya nisikuone tena , nina stahili kufa”

“Wewe , Eujung acha kuwa mjinnga ...”Alifoka na akaendelea kumuomba Roma Eujung asamehewe.

“Mr Roma nitakubali chochote utakachohitaji ili mradi utamuacha Eujung”

“Mimi sijali kama ni mtoto wako au wa nani , anapaswa kufa kwa kumdhuru Yezi”Aliongea Roma kibabe na kufanya jopo lote la watu kupatwa na ubaridi na waliona Roma alipaswa kuacha lipite , isitoshe Yezi amekwisha kupona na Eujung alikuwa akitia huruma.

“Nitakufa kwa niaba ya Eujung , Mr Roma niue mimi , hata hivyo nimeishi maisha marefu lakini Eujung bado ni mdogo”Aliongea Park Juan na kwa wakati huo hakuonekana kama tajiri bali alionekana kama baba.

Roma aliishia kukosa uvumilivu na palepale alimsukuma Park Juan mbali na kisha akampa ishara Clark kumuondoa

“Hebu acha kunichukiza , mtu ninaekwenda kuua hapa ni binti yako na sio wewe”Aliongea Roma na palepale alimsogelea Eujung.

Eujung aliishia kufumba macho yake akikisubiria kifo , alikuwa akijua uwezo wa Roma hivyo aliamini hata kama akileta ukinzani asingeshinda.

“Huwezi kumuua”Sauti ya kikauzu na ya kibabe ilisikika na palepale Kim Jip alikuwa ashamkingia Eujung kwa mbele akimwangalia Roma kwa macho makali kama Cobra.

“Unadhani unaweza kunizuia?”Aliuliza Roma.

“Siwezi”

“Kama ni hivyo unafanya nini?”

“Nimesimama hapa sio kukuzuia bali kukuambia ukweli wote”

“Ukwel?” Aliongea Roma huku akitoa tabasamu la kifedhuli

“Hapana” Eujung alimvuta Kim Jip kumtoa mbele yake.

“Sogea mbele yangu , ananiua mimi na sio wewe , unafanya nini Kim Jip” Aliongea Eujung na palepale Kim Jip alimkumbatia kwa nguvu Eujung na kisha akamwagalia Roma.

“Mimi ndio nimemuwekea sumu Yezi na sio Eujung” Aliongea na kumfanya Eujung kuanza kutoa kilio na kumpiga piga Kim Jip kifuani.

“Kwanini unafanya hivi , nilitaka kufa mimi , kwanini...” Aliongea Eujung mara baada ya Kim Jip kusema yeye ndio muhusika.

Waliokuwa wakiangalia igizo hilo ni kama walishajua nini kinaendelea kati yao.

Kim Yang baba yake Kim Jip alijikuta akipauka uso baada ya kusikia maneno ya mtoto wake , alikuwa katika kiwango cha juu cha hasira na ndani ya dakika

hio hio alijikuta akipoteza fahamu na kusaidiwa na mabodigadi.

“Roma huwezi kumuua mtu asie na hatia , , ninakuamini na nipo hapa kukuambia kwamba mwanamke ninaempenda kwenye maisha yangu ni Ho Eujung , ndio mwanamke ambaye napenda kuishi nae maisha yangu yote , ninaweza kumuua Yezi tena naweza kwenda mbali zaidi na kumua rai Park kwa ajili yake , najua sio fair kwa Yezi lakini sikuwa na chaguo lingine , ninaweza kuwa kichaa au mwanaharamu na nitakubali ilimradi kupigania penzi langu kwa Eujung”Roma aliishia kujiambia yule mtu mkimya leo amekuwa Romantic, alijiambia hakika ogopa sana watu wa kimya wana siri nyingi.

“Lakini ukaguzi na majaribio ya kisayansi yameonyesha yeye ndio kamuwekea sumu, unaongea vipi hapo?”Aliuliza Roma.

“Wewe mwenyewe huoni inashangaza, kama kweli ni muhusika basi angehakikisha anabadilisha mavazi na haachi ushihidi wa aina yoyote , lakini Eujung pengine alipata kichupa ambacho kilikuwa na sumu wakati akiweka sawa suti yangu”Aliongea na kisha alimwangalia Eujung kwa macho ya kimahaba.

“Wewe mwanamke mjinga kwanini ulifanya hivyo , yalikuwa ni maamuzi yangu kuua hivyo nipo tayari kufa lakini nimefurahi , siku zote nilidhania hukunipenda kweli lakini ulichokifanya leo inaonekana nilikudhania vibaya , upo tayari kufa kwa niaba yangu ...nimefurahi”Aliongea

“Mimi sitaki ufe ,, sitaki ufe Kim Jip”Aliongea Eujung.

Wageni waliokuwa wakiangalia waliishia kuwaonea huruma hao wenza, ile hofu waliokuwa nayo ilishapotea na sasa walishangaa drama hizo.

Roma muda huo ambaye alikuwa kimya muda wote aliishia kutoa tabasamu la ushindi na kisha akamgeukia Clark.

“Babe unaonaje maigizo yangu , nadhani ninastahili tuzo...”Aliongea Roma na kumfanya Clark kutoa tabasamu na palepale alimkumbatia Roma na kumpiga busu.

“Upo vizuri... maigizo yako ni ya viwango”

“Hehe... ni kwasababu ya script ulizoniandikia mwenyewe”

Baadhi ya waliokuwa wakielewa kingereza walishangazwa na maneno yao na walionekana kutaka kusikia maelezo yao kwani ni kama vile tukio zima wlaikuwa wakilifahamu.

Clark palepale alitoa chupa yenye kimiminika cha rangi ya pink na kisha akaweka kwenye test tube.

“Nyie watu hakika hamjui Chemistry , hivi mnadhani sumu aina ya Pottasium Cyanide inaweza kugudulika na jaribio la namna hii..”

Maneno yake yaliwashangaza kundi lote ikiwemo Kim Jip na Eujung waliokuwa wakibembelezana.

“Mr Roma ,Dr Clark kwahio unasema... hiki kilichofanyika ni kwa makusudi maalumu?”Aliuliza na kumfanya Eujung nae akili yake kujirudia.

“Kwahio hukugudua chochote wakati wa kunikagua?”

“Ndio , unadhani ni rahisi kuinasa sumu ya Pottasium Cyanide , ukweli ni kwamba Eujung alijimwagia poda ya kawaida tu , nilitaka kumkagua Kim Jip kisayansi zaidi mwishoni lakini mpango wangu ulienda vizuri”

“Kwahio ulijua mimi ndio muhusika tokea mwanzo?” Aliuliza Kim Jip.

“Sikujua kwa uhakika kwani hata Eujung pia nilimdhania ...” Aliongea Roma kisha akaendelea.

“Niliweza kugundua kuna kitu kinachoendelea nyie wawili kwa muda mrefu , pengine mlijua mmejificha vizuri lakini kuna vitu mmeshindwa kuficha , mara ya mwisho wakati nikiishi ndani ya familia ya Yezi , mara baada ya Park Juan kusema anataka umuoe Yezi wewe hukuonyesha ishara yoyote ya kutomtaka kabisa na hukutaka kumwangalia kabisa usoni lakini wakati alipokuwa akipandisha kwenda juu uligeuza shingo na kumwangalia , nilijiuliza kwanini ugeuze shingo wakati humpendi lakini mara baada ya mimi kuangalia nilijua uliekuwa ukimwangalia sio Yezi bali ni Eujung.....” Roma aliendelea kuongea ishara ambazo aligundua kuhusiana na Eujung na Kim Jip kupendana , alikuwa gwiji kwenye mapenzi hivyo ilikuwa rahisi kuusoma mchezo muda mrefu, wanasema mapenzi ni kikohozi na Roma alifanyia uchunguzi kikohozi chao na kugundua.

Roma mara baada ya kugundua viashiria vya kimapenzi kati ya Kim Jip na Eujung palepale

aliwapa kazi watu wake kufatilia taarifa zinazomuhusu Eujung na ndipo alipokuja kugundua mapema kabisa kwamba Eujung ni mtoto wa Park Juan wa nje ya ndoa.

“Eujung nilifahamu wewe ni mtoto wa nje ya ndoa wa Park Juan kwa muda mrefu sana ..”Alimalizia Roma na kufanya kila mtu kushangazwa na maneno y ake yalivyonyooka na kuwa katika mpangilio wa kimatukio na waliishia kumkubali mno.

Hawakuamini mtu mweusi na mkatili kama Roma anaweza kujenga hoja pamoja na kunasa viashiria vidogo namna hiyo na vikawa ukweli.

Ukweli ni kwamba pengine ni kutokana na ubize wa Park Juan ndio maana alishindwa kugundua lakini Kim Jip alikuwa katika penzi nzito na Eujung kwa muda mrefu sana na hata baadhi ya vijakazi walikuwa wakijua hilo lakini walikaa kimya.

“Kama yote hayo uliyajua kwanini bado ukataka nimuoe Yezi , ulipaswa kujua kwamba nisingeweza kumpenda na kumpa furaha”Aluongea Kim Jip.

“Kwasababu Roma alikuamini wewe kama wewe”Alijibu Clark.

“Mimi kama mimi?”

“Ndio wakati wa kipindi kigumu ambacho familia ya Mzee Park inapitia ulisimama imara kupambana na maadui wote wa familia, ulimtunzia siri Eujung kwasababu ya heshima yako kwa Mzee Park Juan. Roma aliokuona kama mwanaume wa ukweli mwenye kifua kipana na huna tamaa, kama tujuavyo ndoa kati yenu ilikuwa ni kwa ajili ya Yezi kupata usalama zaidi pale ambapo angemrithi babu yake, hivyo Roma aliona ni kheri kuolewa na wewe ambaye humpendi lakini huna tamaa kuliko mtu mwingine, lakini kwa bahati mbaya hakuna ambaye alitegemea ungeenda mbali kwa ajili ya mapenzi na kumuwekea sumu Yezi” Aliongea Clark.

“Na kitendo hiki cha kutaka kumuua Yezi siwezi kukuacha hai kwa namna yoyote ile na imenifunza leo hii usimwamini mtu ambaye ashapenda” Aliongea Roma na kisha palepale alisogea.

“Hapana usimuue” Sauti kutoka nyuma ya kundi ilisikika na kufanya watu wote kugeuka na walishangaa kumuona ni Yezi ambaye bado alikuwa amevalia gauni la harusi na alionekana kupona kabisa.

Iliwashangaza kwani alipona kwa haraka sana nje ya mategemeo ya kila mmoja.

* * * * *

Siku kadhaa mbele Kim Jip na Eujung walifunga ndoa rasmi mara baada ya kusamehewa na Yezi.

Roma alitaka kumuadhibu Kim Jip kwa kile kilichotokea lakini Yezi aliingilia kati na kuomba Kim Jip kusamehewa.

Upande wa Yezi alitumia nafasi hio kuweka hisia zake wazi kwamba anampenda Roma kimapenzi na anataka kwenda kuishi nae , maneno ya Yezi yalishangaza kila mmoja na hata Roma mwenewe.

Park Juan alikataa Yezi kujihusisha kimapenzi na Roma kwani tayari amekwisha kuoa lakini Yezi aligoma huku akitumia tukio la mama yake na baba yake lilivyowakuta mpaka kumfanya kuwa yatima na Park Juan mara baada ya kukumbushwa namna alivyovuruga mapenzi ya mtoto wake Park Jooncheni baba yake Yezi alijikuta akijawa na hatia na aliishia kukubali mahusiano ya Yezi na Roma.

Alikuwa na sababu za kukataa Yezi kutojihusisha na Roma moja wapo ni kwamba kama akijihusisha basi angekosa sifa ya kuwa mrithi wake.

Yezi aligoma kabisa kufanywa mrithi wa familia na alichokuwa akitaka ni kuishi karibu na Roma na Park Juan hakutaka kumlazimisha na mwisho wa siku aliamua kumfanya Eujung kuwa mrithi wake ajae badala ya Yezi.

Park Juan hakujali sana watu watakavyomuongelea , ukweli ni kwamba licha ya kwamba hakuwa tayari kumwachia Yezi kuwa mwanamke wa Roma lakini aliamini kuna faida kubwa sana kwa familia yake kuwa na undugu na Roma na mpaka wakati huo alijua ndio atazidi kuogopeka ndani ya Korea kutokana kuwa na Roma nyuma yake.

Roma aliweza kuondoka Korea kabla ya harusi ya Kim Jip na Eujung na hakurudi Tanzania moja kwa moja bali alielekea visiwa vya wafu.

Roma kabla ya kuanza safari aliambiwa Neema Luwazo , Najma, Amina na Lanlan walishafika Visiwa vya wafu kasoro Rufi tu ambaye alikataa

kondoka Tanzania kwa ajili ya kutaka kukaa na mama yake.

Roma mara baada ya kusikia sababu ya Rufi aliotoa ipo kimantiki kwani Bi Wema alikuwa mpweke sana na kama kila mtu aliondoka basi angekuwa peke yake , isitoshe Edna alikuwa mtu bize sana hivyo hakutaka kumlaazimisha Rufi kwenda visiwa vya wafu ili hali hakuwa akijifunza mbinu za kuvuna nishati za mbingu na ardhi.

Upande wa Yezi yeye alibakia Korea na alipaswa kuhudhuria harusi ya shangazi yake Eujung na baada ya hapo kuagana rasmi na familia yake na kuja kuungana na Roma katika visiwa vya wafu na kuanza kuvnua nishati ya mbingu na ardhi kama wengine.

SEHEMU YA 682.

ISLAND X -ZEROS ORGANISATION RESEACH BASE

Ni ndani ya kisiwa X katika makao makuu ya kambi ya kisayansi ya shirika la siri la Zeros Organisation.

Ni siku kumi na mbili tokea kwa Naira kurudi ndani ya kambi hii rasmi baada ya kuondoka kwa takribani mwaka mmoja.

Katika siku zote kumi na mbili Naira alikuwa amepewa uhuru wa kuchagua idara yoyote ambayo atapenda kujiunga nayo kuendeleza misheni za kisayansi ambazo zinaendelea ndani ya hilo eneo.

Kambi hii ilikuwa na maajabu yake , ukiachana na kwamba wafanyakazi wote wanaongia ndani ya eneo hilo hawakuwa wakiruhusiwa kutoka lakini vilevile watafiti wote wlaio kuwepo ndani ya hio ngome muda wote walikuwa waikifanya vitu ambavyo vinasisimua ubongo wao ili kupanua uwezo wao wa kufikiri hivyo ni rahisi kuona mwanasayansi kulala katika chupa kubwa iliojaa maji na kujifunga na vifaa vya kieletroniki , kifufupi ni kwamba maisha ndani ya eneo hilo yalikuwa ni ya kushindana.

Inasemekana kwamba asilimia sabini ya wafanyakazi wote ndani ya hio kambi hawana wazazi wala ndugu katika ulimwengu wa kawaida na walikuwa ndugu wao kwa wao.

Unaweza ukashangaa hili linawezekana vipi lakini ndio utaratibu uliowekwa tokea kuanza kwa kambi hio, kuna binadamu waliopo ndani ya eneo hilo ambao walizaliwa hapo hapo kwa njia za kisayansi, lakini kuna wale pia ambao walizaliwa nje ya eneo hilo ambao walionekana kuwa na uwezo mkubwa wa akili.

Kwa mfano Naira alikuwa ni moja ya watafiti ambao wamezaliwa nje ya eneo hilo na kuonekana kuwa na akili zaidi lakini yeye akiwa tofauti kidogo na wenzake, yeye amezaliwa kwa misheni maalumu ya kisayansi ambayo ilipewa jia la Misheni Pro Human iliofanyika nchini Bolivia miaka mingi iliopita.

Unachopaswa kuelewa hii ni Kambi tu ya kisayansi ambayo ipo chini ya Zeros Organisation.

Kikawaida Zeros organisation haina kabisa makao makuu kwani ni jumuiya ya siri ambayo sio ya rasmi kama ilivyo kwa umoja wa kimataifa bali kama vikao

vikifanyika basi ni kutokana na mpangilio maalumu wa kizamu katika nchi za kila mwanachama, ni kama ilivyo kwa G7 au G20.

Katika siku zote kumi na mbili tokea kufika kwake kila idara ya kitafiti alitumia siku mbili mpaka tatu kusoma taratibu na kujifunza mambo mapya , ilikuwa ni fursa kubwa sana kwa Naira kuliko mfanya kazi yoyote wa kambi hio na yote hayo ni kutokana na kupata ruhusa ya kutembelea kila idara kutoka kwa mkuu wa kambi.

Hatimae siku ya kumi na tatu mara baada ya kutembelea idara zote alikuja kutua katika idara ya PLMC idara ya ufuataliaji wa maendeleo ya Mpango LADO, idara ambayo husimamiwa na Dayana pamoja na Carlos kama wakuu wa kambi.

Naira licha ya kwamba mwanzo alikuwa akifanya kazi chini ya idara hio lakini alitaka kuifanya kuwa ya mwisho kabla ya kupitia idara zote.

Kila mwana idara ambaye alifanya kazi na Naira alikuwa amefurahi sana kumuona kwa mara ya pili , tena sio kufurahi kila mmoja alikuwa akimsubiria kwa hamu kupita kwenye idara yao.

Unaweza ukashangaa kwanini kusumbiria kwa hamu ili hali wapo katika kambi moja ila ukweli ni kwamba kuna sheria maalumu za eneo hilo ambazo hufanya watu wa idara moja kwenda nyingine kutoonana kwa muda wa kila siku ishirini na nne.

Yaanii wana idara wote hujumika mara moja tu ndani ya mwezi ambapo ni kila baada ya siku ishirini na nne , haikueleweka kwanini kuna utaratibu wa aina hii lakini ndio kanuni ilivyokuwa.

Sasa tokea Naira kufika ndio kwanza siku chache zilizopita ndio wana Kambi wote walikutana kwa mara ya kwanza ikimaanisha kwamba baada ya siku ishirini na nne wangekutana tena.

“Welcome back Naira” Aliongea Dr Dayana mara baada ya Naira kufika kwenye idara yao, asubuhi hio na wana idara wote walikuwepo akiwemo Dr Carlos msaidizi pamoja na wanasayansi wengine.

Naira alikuwa amebadilika sana kiumbo , alikuwa amekuwa mtu mzima haswa na alikuwa na zaidi ya miaka therathini kwa wakati huo hivyo ni rahisi kusema alikuwa amekomaa kiakiri.

“Thank you Dr Dayana” Aliongea Naira kwa tabasamu hafifu huku akikumbatiana na mwanamama huyu aliefahamika kwa jina la Dayana mkuu wa idara ya kituo cha ufuatiliaji wa Mpango LADO.

“Naira tulikumisi sana, karibu sana kwenye idara yetu , siku kumi na mbili tokea kusikia uwepo wako ndani ya kambi imekuwa kama mwezi mzima kukusubiri”

“Nashukuru sana Dr Evans niliwamisi sana” Aliongea Naira kwa lugha ya kingereza na palepale mara baada ya kusalimiana na kila mmoja aliongozwa na Carlos na Dayana mpaka kwenye chumba maalumu cha mikutano ambacho kimejaa mitambo ya mawasiliano.

Ijapokuwa Naira alikuwa mwenyeji ndani ya idara hio lakini kutokana na kutokuwepo kwa zaidi ya mwaka mzima basi alipaswa kupewa ushirikiano wa kitaarifa kwa kile kilichojili tokea kuondoka kwake.

Utaratibu ambao ulifanyika katika kila idara ambayo amepita , basi ulipaswa pia kufanyika hata katika idara hio.

Idara ya ufatiliaji Mpango LADO ndio ambayo ilikuwa ikihusika na kufatilia maendeleo ya Agent Code 13, yaani kwa lugha nyingine ni kwamba ni idara ambayo inamfatilia wakala aliekuwa chini ya mpango LADO ambaye hufahamika kwa jina la Agent namba kumi na tatu ,. Huyu ndio Roma Ramoni.

“Dr Evans leo utachukua jukumu la kuwakilisha ripoti ya mpango LADO ulifipofikia na unapoelekea , tunakuamini katika kuongea kwako na kujenga hoja hivyo naamini uwakilishi wako utamfanya Naira kuichagua idara yetu na kufanya kazi na sisi kwa mara nyingine”Aliongea bwana mweusi ambaye ni kiongozi , huyu ni director msaidizi ambaye jia lake ni DR Carlos ni sehemu ya watu weusi wachache ndani ya kambi hio.

Muda huo Naira alikuwa na mchecheto mkubwa , ijapokuwa misheni nyingi ambazo zilikuwa zikifanyika ndani ya kambi hio zilimshangaza lakini alikuwa na mchecheto wa kujua maendeleo ya mpango LADO.

Miaka michache nyuma ndio alietoa pendekezo la namna ya pekee ya kumfanya agent 13 kurekebisha

tabia yake ya kikatili na kuishi maisha ya kawaida ,
pendekezo ambalo lilileta matokeo makubwa
chanya mpaka leo hii , hivyo ni kwamba Naira
aliheshimika.

Naira ndio ambaye alitoa pendekezo la Seventeen
uondolewa katika maisha ya Thirteen ili kupunguza
ile tabia yake ya kimauji , kupumbuka kipindi hicho
Agent 13 alikuwa ni kama mnyama na ilikadiliwa
kwa mwezi alikuwa akiua binadamu kwa wastani wa
watu saba ambayo ni idadi kubwa sana.

Tabia ya agent 13 kuua watu ilikuwa ni athari za
kisaikolojia ambazo zimetokana na sayansi iliopo
ndani ya mwili wake pamoja na ugonjwa uliokuwa
ndani ya ubongo wake. Viongozi wa Zeros
waliwapanikisha wanasayansi hao kuhakikisha njia
mbadala inafanyika ili kumfanya Agent 13 kuacha
mauji na ukatili wake na mbinu nyingi
zilipendekezwa na hakuna ambayo ilifanya kazi na
katika mbinu zote hizo zilikuwa ni zile za
kumrudisha Roma katika maabara na kumwingizia
Chipu kwenye ubongo na wazo hilo lilipingwa vikali
kwani lilikuwa na athari kubwa na hapo ndio Naira
pekee alipokuja na wazo tofauti kabisa na wenzake

wote na wazo hilo ndio ambalo lilikuwa ni la kumtumia agent 17.

“Miss Naira mpaka sasa kuna mabadiliko makubwa sana yametokea chini ya mpango LADO , wakati unatoka mpango LADO ulikuwa kwenye Phase ya tatu na mpaka sasa umefikia Phase namba nne”Aliongea Dr Evans na kumfanya Naira kumwangalia kwa umakini kwa macho ya kutarajia maelezo zaidi.

Katika phase(hatua) namba moja hapa ilihusisha mwanzo kabisa mwa mpango LADO yaani kipindi ambacho ndege ya shirika la M-Airline inapotea hii ndio ilikuwa hatua namba moja au hatua ya kwanza kabisa,hatua ya pili ilikuwa ni ya kimaabara zaidi na hii ilifanyika katika visiwa vya Madagascar na Phase hii ilifanyika mara baada ya Phase namba moja ya kirusi kumalizika , hatua hii ya pili ilihusisha kuwamulika Agent 13 na Agent 17 na mwanga wa jiwe la kimungu sayansi iliopewa jina na Profesa Banosi kama Divine light technology na hatua hii ilikuwa katika mgawanyo wa steji mbili ya kwanza kabisa ni mazoezi ya kijeshi na kininja pamoja na ya pili ni kumulikwa , hatua ya tatu sasa ndio ambayo

Ajenti 13 na Ajenti 17 walipewa nusu ya uhuru wao wa kujiamulia mambo huku tabia zao sikifatiliwa kwa ukaribu.

“Nadhani kila mmoja anaelewa mafanikio ya mpango LADO si tu kwenye kufanikiwa katika majaribio ya kisayansi lakini pia mafanikio yanaandaliwa katika ujumuishi wa matokeo baada ya majaribio ya kisayansi..”

“Evans nadhani ungeenda moja kwa moja katika hatua ambayo mpango LADO umefikia kwa sasa na ni malengo gani yanatarajiwa katika mpango huu” Aliongea Naira na Dr Evans alitingisha kichwa.

“Mpaka sasa mpango LADO umevuka katika hatua ya ufatiliaji wa moja kwa moja kupitia mitambo mpaka kuwa katika ufatiliaji wa kijasusi”

“Unamaanisha kwamba hakuna mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Ajenti 13 na kituo chetu cha ufatiliaji?” Aliuliza Naira kwa kingereza.

“Ndio” Aliongea na palepale aliwasha mtambo ambao siku zote ulikuwa ukitumika kumfatiliaji utendaji kazi wa mwili wa Ajenti 13, siku za nyuma mtambo huo ulikuwa ukionyesha data ambazo zinacheza cheza

lakini kwa kipindi hicho hakukuwa na dalili yoyote yaani kwa haraka haraka ni kwamba mtambo huo uliandika ‘No Signal’

Jambo lile lilimfanya Naira macho yake kuchanua na alionyesha tabasamu hafifu.

“Madam hatua hii inatafsirika vipi?” Aliuliza Naira akimwangalia Mama mtu mzima ambaye hufahamika kwa jina la Dyana.

“Mpaka sasa hatua hii inatafsirika kwamba PLMC haina access ya moja kwa moja na Agent 13 na swala hili linahamia moja kwa moja chini ya kitengo maalumu cha kijasusi kilichopo chini ya Dhoruba nyekundu , kama aliyyosema Evans Mpango LADO kwasasa upo katika hatua ya kijasusi zaidi kuliko ‘remote monitoring’”

“Kama mpango huu upo katika hatua hii ni kazi gani ambayo imebakia chini ya PLMC?” Aliuliza Naira.

PLMC ni kifupi cha Project Lado monitoring center

“Ijapokuwa kwasasa mpango LADO upo katika hatua ya kijasusi zaidi kuliko ya kisayansi haimaanishi kwamba idara yetu ndio inafungwa kutokana na kukosekana kwa majukumu , kama alivyokwisha

kusema Dr Evans kwa sasa tupo katika hatua ya nne lakini kuna hatua ya tano na ya sita, katika hatua hizi kinachongojewa ni kizazi kinachofuatia”

“Unamaanisha watoto watakaozaliwa na Agent 13?”

“Ndio Naira ,hio ndio itakuwa hatua ya tano ya mpango LADO ambayo mpaka sasa ipo nusu kufikiwa”

“Unamaanisha nini kusema nusu kufikiwa?”Aliuliza Naira huku akionyesha shauku na palepale Carlos alimpa ishara Evans kuendelea.

“Dr Naira , huyu ni Lanlan Ramoni Kweka ni mtoto wa kwanza wa Agent 13 na Agent 17, hizi ndio taarifa ambazo zinamuhusu Lanlan mpaka sasa kuanzia maendeleo ya ukuaji wake, tabia yake na utimamu wa akili yake”Aliongea na kisha alipatiwa kishikwambi kilichokuwa na chata ya Zero na kuanza kusoma na Naira alijikuta akisisimkwa na mwili.

“*Kwaninin Athena hakunielezea kuhusu kuwepo kwa Lanlan?*”Ni swali ambalo liliibuka palepale katika kichwa cha Naira.

“Umesema hatua ya tano ipo nusu kufikiwa , nataka maelezo ya kutosha kuhusu hili”Aliongea na

palepale Dr Evans ni kama alisubiria swali hilo kwani alitoa tabasamu na kuanza kuelezea maisha ya Roma kuanzia kufika chini Tanzania namna ambavyo amekutana na Edna na wanawake wengine.

Ilikuwa ni taarifa ambayo alikuwa akiijua nusu yake lakii alishangazwa mara baada ya kuona Roma alikuwa na kundi kubwa la wanawake tena akiwemo rafiki yake wa utotoni Dorisi.

Naira alisisimkwa na mwili palepale na alishajua ni kipi ambacho kilikuwa kikitarajiwa kwa haraka haraka kilichokuwa kikisubiriwa katika mpango huo ni watoto ambao Roma atapata kupitia wanawake hao.

“Manaamii vipi watoto watakaopatikana kupitia hawa wanawake wataweza kuwa na uwezo mkubwa kuzidi huyu Lanlan?”

“Matarajio yetu ni makubwa sana kupitia watoto watakaopatikana, mpaka sasa tuliweza kufatilia kwa karibu sana namna ambavyo Agent 13 alivyoweza kujiondoa katika mifumo yetu ya kiufatiliaji, ijapokua hakuna maelekezo sahihi ya kisayansi lakini inaonekana mbinu ambayo amejifunza chini ya Master Tai Chi ndio sababu kubwa, mpango wetu

mwanzoni ni kumfanya kuweza kuzielewa kanuni za anga lakini akachagua mbinu nyingine ya ajabu, ni kwamba mwili wake umepitia steji ya ‘purification’ na ndio iliosababisha kukosa mawasiliano nae ya moja kwa moja kutokana na sayansi ya ufatiliaji kufutika kwenye mwili wake, hizi ni taarifa za mwisho ambazo tuliweza kufatilia kuhusu mwili wake” Aliongea na kisha palepale alitoa ripoti nyigine na kumpatia Naira.

“Virusi ambao waliingizwa katika mwili wake walikuwa na kazi kubwa ya kupitia mabadiliko pale anapokuwa ni mwenye hasira lakini tokea mwili wake kutawaliwa na nguvu isiokuwa ya kawaida, virusi wote wamekosa utawala wa seli za mwili na kubakia kama chembe chembe ndani ya mwili wake , dalili pekee ambayo inafanya kazi katika mwili wake ni nguvu ya mwanga wa kiuungu ambao alimulikwa nao na huu hujidhihirisha kupitia macho yake”

“Naona hapa faida kubwa ambayo ameipata kupitia mpango LADO kwasasa ni kuwa na mwili usio wa kawaida lakini nguvu zake hazitegemeanni kabisa na mpango LADO ni hatua nzuri ambayo amefikia , vipi

lakini kuhusu uvimbe uliopo kwenye ubongo wake?”

“Mpaka sasa hatuna taarifa zake kutokana na mtu ambaye huhusika katika kumpima ni princess Clark Stephanie na kutokana na teknolojia kubwa ya kimitambo anayotumia tumeshindwa kudukua taarifa zake” Aliongea na kumfanya Naira kuvuta pumzi kidogo na kuwaza jambo.

“Sio Ajent 13 tena bali ni Roma Ramoni kwa jina lake , amepiga hatua kubwa lakini je anaelewa mipango ya Athena, ninapaswa kutengeneza njia ya kufanya nae mawasiliano kwa namna yoyote ile, hii sio kwa ajili yake tu lakini pia kwa ajili yangu na ulimwengu wote, lakini Athena anaonekana kuwa na wasiwasi juu ya mtu alimrithisha Roma uungu wake... hii inamaana gani?” Aliwaza Dr Naira kwa muda mrefu.

Alikuwa akijua Athena ana wasiwasi kabisa juu ya Hades wa Zamani na alishindwa kujua wasiwasi wake upo kwenye nini.

“Kwanza niseme kwamba nimferahishwa na kazi kubwa ambayo idara ya PLMC imefanya kwa kipindi chote ambacho sikuwepo hii inanipa shauku ya

kutaka kujua nini kinafuatia katika hatua ya tano na sita ya mpango LADO ila niseme kwasasa nimevutiwa zaidi na Project ya Quantam Nexus na Quantum Horizon hivyo nitahama idara”Aliogea na kufanya kila mmoja kuwa katika mshangao lakini kwa wakati mmoja wakiingiwa na huzuni.

Quantum Nexus na Horizon ndio idara kubwa za kitafiti ambazo pia zilikuwa zikiendelea chini ya Zeros organisation.

Kauli ya Naira iliwafanya kujawa na huzuni kwani ilimaanisha kwanzia siku hio hatokuwa tena chini ya idara ya PLMC bali anakwenda kujiunga na idara ya utafiti wa kisayansi wa teknolojia ya Quantam mechanic.

SEHEMU YA 683.

Warembo wa Roma waliokuwa wakiishi ndani ya visiwa hivyo ndio waliokuwa na jukumu la kuwapokea wenzao katika uwanja wa ndege.

Ilikuwa ni kipindi cha hali ya hewa ya unyevunyevu ndani ya eneo lote la mwambao wa bahari ya Mediterranean hivyo ilifanya kisiwa kupendeza zaidi kwani ni hali ambayo ipo katikati haikuwa ya joto sana wala ya baridi sana kwa mwezi huo wa kumi na mbili kuelekea mwezi wa kwanza.

Roma alikuwa amemlisi sana Rose na warembo wengine kwani hakuwaona kwa kipindi kirefu na mara baada ya kufika alijikuta akiwakumbatia na kuongea nao maneno matamu ya kuwafurahisha.

Upande wa Rose na Magdalena walikuwa wamepiga hatua kubwa sana katika mafunzo ya mbinu hizo za

kijini walikuwa katikati mwa levo ya Nafsi na hata mahusiano kati yao yalibadilika, ile hali ya ashiki ya kimapenzi waliokuwa nayo mwanzo ilibadilika mno.

Kadri ambavyo uwezo wa mwanamke anavyopanda levo na tamaa ya kimapenzi hushuka zaidi na zaidi na upendo unaobakia sio ule wa kingono zaidi bali ni ule ambao hauelezeki kwa maana nyepesi.

Roma ni kama vile amejandika katika mioyo ya wanawake hao kwa karamu ambayo wino wake ni ngumu kufutika.

Ilikuwa ni kwa ghafla sana tayari kisiwa kilikuwa na wanawake kumi wa Mfalme Pluto , hali hio iliwafanya wakazi wa eneo hilo kuvutiwa sana na picha hio , hakukua na sheria ya kitamaduni ndani ya hivyo visiwa na kilichohesabika ni kwamba wanawake hao ni wa mfalme Pluto na wanapaswa kuheshimiwa , huo ndio ukweli ambao raia wa visiwa hivyo walipaswa kuelewa.

Ilikuwa ni kwa bahati nzuri kwamba wanawake hao hakuna ambaye alikuwa na tabia mbaya au hasira za kutumia nguvu ya Roma vibaya , kwa zaidi sana ni Mage ambaye alikuwa mtu wa vitendo zaidi kwani

ndani ya muda mchache aliofika alikuwa ashaanza kufahamiana na wakuu wa vitengo wote waliokuwa chini ya Roma na kujua ngazi zao na madaraka yao lakini hata hivyo wote walimpa heshima yake na hawakuchukizwa na maswali yake mengi zaidi ya kutoa ushirikiano pale wanapotembelewa.

Ujio wa Lanlan ndio ambao ulikuwa ni wa kivutio zaidi ndani ya visiwa hivyo kwasababu kila mtu alijua huyo ndio mtoto wa Seventeen na Roma na uzuri ni kwamba asilimia kubwa walikuwa wakimjua Seventeen kwani alishaishi ndani ya visiwa hivyo na wakampa heshima yake na alikuwa na mchango mkubwa lakini pia walijua ni nafasi gani aliokuwa nayo katika maisha ya Roma.

Hivyo kila mmoja alipenda kumuona Princess Lanlan na kujenga nae ukaribu kwa kumsifia hivi na vile.

Lanlan alijikuta kwa muda mfupi sana anakuwa na wajomba , mashangazi na mababu na alishindwa kujizuia na kujikuta ni mwenye furaha kwani wale aliowaita mababu walimfurahisha zaidi kutokana na hongo ya chakula walichokuwa wakiandaa na pia burudani waliokuwa wakimuonyeshea.

Ki ufupi Lanlan ndio aliekuwa bize zaidi kuliko wote na ilimfanya kusahau kwa muda kufanya mazoezi kiasi cha kuhofia baba yake kumfokea.

Lakini kitu kungine ambacho kilimfurahisha Lanlann ni uwepo wa bahari ambayo hakuwa akiona mwisho wake , bahari ambayo ilimruhusu kuogelea muda wote na kulikuwa na watoto wengi ambao alikuwa akicheza nao bila ya kumhofia.

Watoto waliokuwa akicheza nao wazazi wao wenyewe hawakuwa wa kawaida na walikuwa na vyeo hivyo ni kama ujasiri wao wamerithisha watoto wao na hawakuwa wale watoto legelege , walikuwa ni watoto ambao wana aina ya mazoezi kulingana na umri wao,

Tanzania watoto ambao Lanlann alikutana nao shuleni asilimia kubwa ni wale wadhaifu wadhaifu na wazembe ambao wamekaa ki uwoga woga na kumuogopa lakini watoto wa kisiwa hicho walikuwa ni wa tofauti sana na hili ndio ambalo lilimfurahisha Lanlan na alifurahi hata pale alipopigwa makofi mara baada ya kumuua Papa na kumburuza mpaka nchi kavu.

Upande wa wanawake wa Roma walijua kabisa mume wao amewaleta katika visiwa hivyo sio kula bata bali kujifunza hivyo hawakutaka kumkatisha tamaa , walifikia hadi hatua ya kushindana wao kwa wao.

Isitoshe Rose , Magdalena na Sophia walikuwa na levo za juu zaidi katika mafunzo hayo na ndio ambao walishindana zaidi wao kwa wao na kila mmoja alitaka kumshinda mwenzake na ndio maana walitumia kila maelekezo ambayo Roma huwapatia.

Katika siku ya kwanza ambayo Roma alifika hakutaka hata kwenda kutembelea marafiki na alijichimbia katika chumba cha ardhi katika ngome yake na kuanza kutengeneza vidonge vya kijini.

Alikuwa na lile tunda moja tu la damu na hakujua ni vidonge vingapi ambavyo angetengeneza hivyo alitumia umakini mkubwa sana katika utengenezaji hili asije kuharibu.

Roma alitumia kila mbinu ambayo ilikuwa kwenye andiko la malkia wa tushani alilopatiwa na Aoiline katika ulimwengu wa majini pepo na aliishia kujawa na shukrani kubwa.

Kitendo cha Roma kufanikiwa kutengeneza kidongea daraja la kwanza kiliwafanya hata Rose na Magdalena na Sophia waliokuwa wakivuna nishati katika kilele cha mlima Volcano kuhisi nguvu yake na kukimbilia ndani ya ngome.

Roma ile anatoka katika chumba cha siri cha utengenezaji vidonge aliwakuta warembo hao wakisubiria nje kwa shauku kubwa na aliishia kutoa kicheko kutokana na macho yao yalivyojaa shauku na tamaa.

“Naona mmekuja kwa haraka sana lakini siwezi kuwapatia hivi vidonge , ni vya watu ambao wanataka kuingia katika levo ya Nafsi na nyie tayari hivyo mkae pembeni”

“Shiii.. mimi na Magdalena hatuhitaji sana , tulitaka kuona tu vinavyoonekana” Aliongea Rose ambaye urembo wake umeongezeka mara tano zaidi , ni dhahiri kama angetia mguu ndani ya Tanzania wanaume wangepanga mstari kuomba hata namba alikuwa sio wa kawaida na kama una nguvu kidogo sana za kiume basi ukimwangalia ni kama vile uso wake unabadilika badilika kutokana na kuzingirwa na nguvu ya mbingu na ardhi.

Haikuwa kwa Rose tu hata kwa Magdalena alikuwa na mabadiliko makubwa saa ya kimwili na moja wapo ya faida ya nguvu za kijini ni kwamba zinakuja na aina ya marashi asili ambayo hayaelezeki , yaani ni aina ya marashi ambayo haihitaji kujipuliza.

“Umepauka uso , unaonekana umechoka sana kwa kutumia nguvu ya moto mweupe kutengeneza vidonge kwa siku tatu mfululizo”Aliongea Rose huku akishika shavu la Roma kimahaba huku macho yake ni kama yamejaa machozi lakini ukweli nin kwamba hayakua machozi bali nguvu ya kijini ndio ilifanya macho kuwa kama yamejaa maji na kulegea.

‘Nimepoteza nguvu kidogo tu lakini nitakuwa sawa kama utaniruhusu ninyonye asali yako kwa dakika kadhaa babe Rose”Aliongea Roma kama kawaida yake huku akitoa tabasamu la kifedhuli.

“Hebu achianeni kwanza , nataka kujua ni vidonge vingapi umetengeneza”Aliongea Magdalena huku akimvuta Rose kwa nguvu.

“Haha.. Magdalena wako ni wivu kama na wewe unataka si ujiunge upigwe busu”Aliongea Rose akimtania Magdalena na kumfanya kumpotezea.

“Nimetengeneza vidonge kumi tu kwa kutumia lile tunda la damu la finiksi , nyie wawili pamoja na Sophia hampaswi kupewa , nitawapa ambao wanapaswa kuingiakatika levo ya Mzunguko kamili na levo ya nafsi”

“Vinatosha hivyo kabisa na vinaonekaa kuwa na nguvu kubwa kutokana na msisimko wake , sisi hatuna tatizo ukiwapa wengine” Aliongea Magdalena lakii akiwa na sura ya huzuni.

“Magdalena kwani kuna utamu gani kuhusu vidonge , hupaswi kuwa na huzuni , mimi mwanaume wako nitakulisha kitu kingine tofauti na vidonge...” Aliongea Roma huku akikodolea kifua cha Magdalena kwa macho ya kifisi na kauli yake ilimfanya kuwa na aibu na kumwangalia Roma kwa macho ya hasira.

Baada ya kuongea na Magdalena na Rose kwa muda Roma aliwaita wanawake wote kurudi katika ngome hio , ilikuwa ngome kubwa mno na kila mmoja alikuwa na chumba chake kikubwa tu lakini ajabu ni kwamba licha ya Roma kuwaachia uhuru wa kuchagua hakuna ambaye alichagua chumba kikubwa zaidi cha hadhi ya juu ambacho Roma mara ya kwanza alijaribu kulala na Edna na akagoma.

Roma mara baada ya kuwakusanya kwenye meza alitoa kifaa ambacho amehifadhia vile vidonge.

Neema Luwazo , Amina , Mage, Najma , Nasra , Dorisi na Clark wote walichukua kimoja kimoja na kwasababu Yezi ndio kwanza ameanza kujifunza basi hakupaswa kuchukua na Roma alimuhifadhia hivyo katika vidonge kumi vilibaki viwili tu ambavyo Roma alipanga kimoja kingekuwa ni cha Edna.

Lakini Roma hakuwa na mpango wa kumpa Edna kwa haraka kutokana na vita baridi inayoendelea.

“Kwa taarifa yenu tu , hiki kidonge ijapokuwa kina nguvu sana lakini lazima kutakuwa na maumivu makali sana ya kuvumilia baada ya kukimeza hivyo kama unaogopa basi usimeze isitoshe mimi sio kama wale Master wakali , nataka kuwaona mkiwa salama hivyo haina haja ya kuharakisha , kama ukishaingia levo ya mzunguko kamili haina haja ya kuharakisha kuingia levo ya nafsi”

“Unaongea kama vile unatuona sisi ni watoto wa miaka mitatu , hivi unajua ni maumivu gani wanawake wanapitia wakati wakifanya upasuaji wa sura na shepu ili kuwa warembo , mwanamke yoyote

anaweza kuvumilia magumu yote ili mradi tu matokeo awe mrembo”Aliongea Neema.

“Sio hivyo , ninachomaanisha ni kwamba ijapokuwa ni kweli kuna maumivu mtapata lakini sijui ni maumivu ya aina gani kwani mwenyewe sijawahi kujaribu ., sitaki kuona mkipitia wakati mgumu”

“Angalau una dhamiri ya kueleweka , hivyo hebu nikutoe wasiwasi kwa kukuambia mimi nitakuwa wa kwanza kujitoa kafara kumeza hiki kidonge”Aliongea Afande Mage na palepale alichukua kidonge chake na kukimeza palepale na kufanya wote kumkodolea macho.

Alitaka kuwa wa kwanza katika majaribio na alikuwa jasiri kiasi cha kuwafanya wengine kuonyesha kumpenda.

Magdalena alitaka kumzuia dada yake lakini alikuwa amechelewa kwani kishapita kwenye koo tayari na aliishia kuwa na wasiwasi tu ya kile ambacho kinakwenda kumtokea na hakutaka aendelee kubakia hapo kwani alimbeba na kuondoka nae na kwenda ndani ya vyumba vya chini ya ardhi.

Roma na yeye alifatisha huko huko akitaka kujionea kama Mage atafanikisha kutumia nguvu yote ya kidonge hicho na kupanda levo.

Ndani ya chumba Mage alikuwa amekalishwa kwenye Sofa na alikuwa akitokwa na jasho ambalo sio la kawaida huku mwili wake ukitoa mvuke ambao harufu yake haikuwa nzuri kabisa ilikuwa ni kama vile hajaoga muda mrefu lakini Roma aliweza kugundua ni hatua ya kwanza ya kidonge hicho kusafisha mwili kabla ya kuruhusu nguvu nyingine kumvaa lakini wakati huo mishipa ya damu ilikuwa imetanuka sana kwani hata uso wake ulikuwa ukionekana michirizi ya mishipa ya damu.

Wakati huo alikuwa ashapoteza fahamu na Magdalena alitaka kumsaidia dada yake lakini Roma alimzuia.

“Usimguse kabisa na umuache , hatua ya kwanza ya kusafisha mwili ni ngumu kidogo na ndipo maumivu yalipo , kama asipofanikiwa kuvumilia yeye mwenyewe basi itakuwa rahisi kupoteza uwezo wake huko mbeleni”

Mage alikuwa kama taa ya balbu ambayo inakaribia kupasuka kwani alikuwa akirejewa na fahamu na kisha zinapotea tena pale maumivu yanapomzidia na mara ya mwisho kabisa mara baada ya fahamu kumrejea hakupoteza fahamu tena na aliishia kung'ata meno na kukunja ngumi huku akitokwa na mvuke wa ajabu mno na kubadilisha hali ya hewa ya chumba.

Nusu saa mbele alianza kuota vipete vikubwa ambavyo vilikuwa na damu nyeusi na hapo ndio maumivu yalipozidi kiasi cha kumfanya kutetemeka lakini hakupoteza fahamu tena na vipete vile vilikuwa vikiota na kupasuka vyenyewe.

Watu wote walikuwa wakimwalia mpaka lisaa linapita walijikuta wakishangazwa na nguvu za mbingu na ardhi ambazo zilikuwa zikimwingia Mage na jambo hilo liliwashangaza wote na Roma alijiambia alifanya la maana kuwaleta huku kufanyia mazoezi kwani nguvu hio kwa hakika lazima ingewaamsha majini.

Baada ya maumivu yaliidumu kwa saa moja na nusu hatimae mvuke uliisha kwenye mwili wa Magdalena na ngozi yake ilianza kujiotesha upya na kubakia na

magamba magamba ambayo yalikuwa yakimtoka kwa kugusa tu na mkono , ilikuwa ni ajabu kweli.

“Haha... Mage tayari amefanikisha kunyonya nguvu ya kidonge na kilichobakia hapo ni kuingia katika tafakari nzito ya kuweza kupata ufunuo wake na kuingia katika levo ya Nafsi” Aliongea Roma huku akijipongeza na mara baada ya kuona ufanisi wa vidonge hakuona haja ya kuwazuia wengine kutokuvimeza.

Usiku chakula kiliandaliwa kama kawaida na mpishi wa kimataifa ambaye alipewa ajira kabisa kwa ajili ya kazi hio.

Lanlan alikuwa akila zaidi ya vile alivyokuwa akila alipokuwa Tanzania na mashavu yalizidi kumtoka lakini licha ya hivyo Roma aliamini kadri ambavyo atajifunza basi mafuta ya mwili wake yangejiwianisha kwenye mwili wake na kuwa na mwonekano mzuri zaidi.

“Daddy lini tunarudi?” Aliuliza Lanlan ambaye alikuwa amekaa pembeni.

“Umechoka kukaa huku?”

“Sijachoka lakini Lanlan anataka kwenda shule”

Ukweli ni kwamba licha ya mzingira ya hapo kuwa na marafiki wengi ambao anacheza nao lakini kuna aina ya michezo hawakuwa wakicheza kwani wengi wao walikuwa ni wasichana ambao wamekaa kitomboy kitomboy na waliishia kumwita Princess tofauti na Lanlan jina ambalo hakuwa akilipenda.

Bado siku tatu mpaka likizo kuisha , nitakurudisha kabla ya hio siku”Aliongea Roma.

“Hata mimi pia nitaondoka”Aliongea Nasra lakini muda huo huo wote walikatishwa na kuingia kwa Mage ambaye alikuwa bado hajatoka kwenye chumba cha ardhi , muda huo alikuwa amebadilika na ngozi yake mpya ilishajitengeneza na yale mabaka mabaka kama nyoka anaejichuna yashaisha na sasa alikuwa ameoga na kupendeza.

“Yuko mwishoni mwa levo ya Mzunguko kamili”Aliongea Roma na kuwafanya Magdalena na Rose kuangaliana , ufanisi wa kidonge ulikuwa mkubwa kuliko walivyotarajia.

Mage hakujali walivyokuwa wakimwangalia na alikimbilia chakula na kuanza kukifakamia na alipiga

sahani tatu mfululizo kiasi cha kumhuzunisha Lanlan maana alizidiwa.

Usiku Roma alijaribu kutafuta sasa watoto kwa Magdalena na Rose lakini hata hivyo hakuwa na matarajio makubwa kwani kulikuwa na gepu kubwa hivyo ilikuwa ni kwa kubahatisha tu hivyo ilikuwa ngumu kubeba uja uzito.

Siku iliofuata Najma , Clark , Amina , Neema , Nasra na Dorisi wote walimeza vidonge kwa wakati mmoja na mpaka inafika mchana wote waliweza kupita hatua ya maumivu ya mwili kujisafisha kasoro Clark tu ambaye alikuwa amejifungia kwa muda mrefu sana kiasi cha kuwafanya wengine kuwa na wasiwasi na kutaka kumshitua lakini Roma aliwazuia.

Siku ya kwanza ilipita bila ya Clark kutoka na Roma hakumgusa ili mradi alijua mwili wake upo sawa na Roma alishangazwa na jambo hilo lakini alijiambia angefahamu zaidi atakavyoshituka.

Roma siku iliofuata alianza uwafundisha warembo hao mapigano ya kijeshi na kimapigano kujiweka sawa.

Kwa jinsi ambavyo walikuwa wakijifua ni kama vile muda wowote Roma anakwenda kuingia vitani baada ya kuhitimu mafunzo.

Mpaka inakuja kufika usiku ndio sasa Roma aliweza kuhisi msisimko usio wa kawaida na hakuwa yeye tu hata Magdalena na Rose wote waliweza kuhisi msisimko huo na hapo ndipo walipojua Clark alikuwa ameingia kwenye levo ya nafsi jambo ambalo lilishangaza kila mmoja , ilikuwa ni maajabu kwani Clark alikuwa ameingia levo ya Nafsi ndani ya masaa ishirini na nne tu na nusu.

Ijapokuwa Sophia aliingia ndani ya levo ya Nafsi kwa spidi lakini yeye alikuwa na msaada kutoka ka Aoiline lakini Clark peke yake aliingia katika levo ya nafsi kwa msaada wa kidonge tu.

Wakati Clark alipotoka nje alikuwa kama vile ni Aphrodite mungu wa kizazi , labda ni kwasababu alikuwa ndio mzungu pekee katika kundi la wanawake wa Roma.

Kila mmoja alitaka kusikia siri ya Clark kuweza kutoboa ndani ya siku chache na hapo ndipo walipomsikiliza kwa umakini kuhusu ufunuo aliopata

na kwa maelezo yake anasema alijaribu kulinganisha nadharia ya Einstein kati ya anga na muda , yaani kwa lugha nyepesi ni kama Clark alikuwa ameiga namna kanuni za anga zinavyotumika na ndio alipoweza kupatwa na uelewa wa haraka

Mbinu ya Clark ilikuwa ni ya ajabu mno na hata Roma mwenyewe alishindwa kuielewa na alijua Clark anaweza kuwa tishio zaidi kuliko wengine wote.

Siku chache mbele Sophia ambaye alikuwa Italy kwenye show aliungana na Roma katika visiwa vya wafu na iliandaliwa tafrija ndogo ya kumpongeza kila mmoja kwa mafannikio, wakati wengine wote wakiwa wamefikia levo ya mzunguko kamili Clark , Sophia , Rose na Magdalena walikuwa washaingia katika levo ya mwishoni mwa mzunguko kamili na muda wowote wangeweza kutoboa , ilikuwa ni juhudi kubwa.

Baada ya tafrija hio Roma aliwaambia wanaotaka kurudi bongo wajiandae na safari na wanaobaki wabaki lakini wote hakuna ambaye alitaka kuondoka kabla ya kufikia levo ya nafsi kasoro kwa Nasra tu ndio alitaka kurudi.

Roma sasa mara baada ya kuona mafanikio ya warembo hao ukweli ni kwamba alifikiria muda wa kutafuta mbinu ya kufanya wawe huru licha ya kuwa nguvu za kijini baada ya kufika levo ya nafsi na aliona mbinu pekee ni kuzidi kuvuna nishati ili kuwa na nguvu kubwa ya kwenda kubadilisha sheria walizoweka majini na kuwafanya warembo wake wawe huru kwenda wanapotaka.

Najma akiwa visiwani alijulishwa kuteuliwa na kuwa afisa habari na msemaji mkuu wa wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki na alipaswa kuripoti Dodoma siku kumi zijazo hivyo aliungana na rafiki yake Nasra na Roma kurudi Tanzania.

Roma ijapokuwa alishangazwa na chaguo la Najma kujiingiza kwenye siasa lakini hakutaka kutoa dukuduku isitoshe hakuona tatizo kwa mtu kutaka kuwa na nguvu ya kimadaraka , alijiambia ili mradi atakuwa na furaha basi atamsapoti.

Roma mara baada ya kufika Ununio ilikuwa ni usiku tayari na walishangaa kukuta nyumbani kwa Nasra taa inawaka kwa ndani kwani walitegemea Qiang anaishi kwa Bi Wema.

Roma alijiuliza ni nani yupo ndani na wakati huo alikuwa amemshikilia mkono Nasra kwa mkono wa kushoto na Lanlan mkono wa kulia.

“Roma mwanangu naona hatimae umerudi”Sauti iliweza kusikika mara baada ya mtu kutoka nje na palepale Roma aligundua alikuwa ni mama yake Blandina.

Na alimwangalia Roma kwa umakini kama vile kuna kitu anatafuta na aliridhika kuona hana tatizo lolote.

“Mama kwanini upo huku , umefika lini?”Aliuliza Roma kwa mshangao.

“Kwanini unaniuliza hivyo au siruhusiwi kuja sehemu anayoishi mwanangu ?”Aliongea Blandina akionyesha hali ya kutoridhishwa na swali la Roma na palepale alimsogelea mjukuu wake na kumbeba juu juu.

“Jamani Lanlan ulikuwa ukila nini huko visiwani , mashavu yameongezeka”Aliuliza na Lanlan aliishia kucheka cheka na kuishia kuita bibi tu.

Baada ya kuingia ndani Blandina aliongea kidogo na Nasra kisha akakaa chini na kuongea na Roma.

“Mama umemaliza maswala yako , uliniambia kuna mamabo unashughulikia nje ya nchi mara ya mwisho?”

“Ndio maana nimerudi , nimeamua kurudi sasa kuishi huku,Roma nimesikia habari zako nikiwa huko , niliambiwa uliweza kupunguza nguvu ya familia ya mzee Sharif”Aliongea

“Umesikia wapi?”

"Baba yako ndio kaniambia , anaweza asikuambie moja kwa moja lakini amekusifia sana"Aliongea Blandina.

"Inaonekana ukaribu wenu umeongezeka mama??"Aliongea Roma huku akitoa tabasamu.

"Nina wasiliana nae kwa ukaribu kwa ajili yako , nataka ifikie hatua muwe mnaelewana , Najma amepata nafasi ndani ya wizara ya mambo ya nje inaonekana baba yako anaonyesha juhudi kwa namna yake"Aliongea na kumfanya Roma kusbindwa kuongezea, hakujali sana kuhusu Senga baba yake alijiambia ilimradi hamchokozi basi.

"Roma wewe na Edna mmefikia hatua gani ,
nimemuuliza Qiang lakini anaonekana hajui
chochote , hujafanikiwa kumlegeza japo kidogo??"

"Hakuna kinachoendelea nadhani ndio muda
muafaka wa kusaini makaratasi ya talaka"

"Huyu mtoto ni kama baba yake tu ana kiburi mno ,
halafu Jeremy wala hajali kinachoendelea" Aliongea
huku akimsukumia lawama raisi jeremy.

Upande.wa Blandina alikuwa haridhishwi na tabia ya
Edna na siku zote alitamani hata Nasra ndio awe
mke wa Roma.

Upande wa Roma alijiambia hata kama Edna
anakwenda kutalakiana nae asingekuwa na haja tena
ya kuoa mwanamke mwingine.

"Mama mimi sina mpango wa kuchukua hatua kutoa
talaka labda alazimishe , kwasasa bado namchukulia
kama mke wangu kisheria na mara nyingi hisia zangu
zinaniambia Kuna.sababu ya kipekee ambayo ina
msumbua Edna ndio maana anashindwa kuniambia
nishaamua tayari hata kama tutaachana lakini bado
nitendelea kumjali"

" Roma usilazimishe, mimi kwa maoni yangu kuna sababu mbili ambazo zinamfanya mwanamke kukuacha ya kwanza ni kwamba hakupendi kabisa na nyingine anaweza akawa anakupenda lakini humpi mapenzi ya kumtosheleza, haijalishi ni ipi sababu yake ni ngumu sana kurudisha mawazo yake nyuma kama tayari ashaamua"Aliongea Blandina.

.....

Siku iliofuata Lanlan alifungua shule rasmi na bibi yake ndio alimpeleka na upande wa Roma alienda kumtafuta Rufi maana ndio pekee hakuwa ameenda visiwa vya wafu , siku nzima walishinda pamoja na jioni Roma alirudi na moja kwa moja alienda nyumbani kwa Edna.

Alimkuta Bi Wema peke yake na Edna hakuwa amerudi kutoka kazini na Roma aliona asubiri kwani ndio ulikuwa muda wake wa kurudi.

Nusu saa tu baadae hatimae Edna aliwasili akiwa ndani ya gari mpya nyekundu aina ya Bentley , ilikuwa gari nzuri mno ambayo iliendana na muonekano wake.

Roma aliekuwa amekaa nje kwenye bustani aliishia kuikodolea macho gari hio mpaka ilipoegeshwa na palepale Edna alitoka.

Muonekano wake ulikuwa ni ule wa ki'superwoman' na alikuwa amebadilika zaidi na zaidi kwa jinsi alivyokuwa akionekana, alikuwa akijiamini mno na hakuwa yule Edna mnyonge mnyonge.

Licha ya kumuona Roma lakini ni kama vile hakuwa akimjua na ile anataka kuingia ndani Roma alifutika alipokuwa amesimama na kuibukia mbele yake na kumzuia.

ITAENDELA.